



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI
WANAWAKE WA VITI MAALUM

Dodoma, 30 Januari, 2024


Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha jana tarehe 29 Januari, 2024, imewateua Madiwani Wanawake wa Viti Maalum watano (5) kujaza nafasi wazi katika Halmashauri tano (5) za Tanzania Bara. Uteuzi huo umezingatia matakwa ya kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292.

Uteuzi wa Madiwani hao wanawake wa viti maalumu umefanyika baada ya Tume kupokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa mujibu wa kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292, aliitarifu Tume juu ya uwepo wa nafasi wazi za madiwani wanawake wa viti maalum katika Halmashauri tano (5) za Tanzania Bara. Nafasi hizo zimetokana na vifo vya Madiwani hao wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Tume baada ya kupokea taarifa hiyo ilimfahamisha Katibu Mkuu wa CCM juu ya uwepo wa nafasi wazi. Chama hicho kiliwasilisha majina ya wanachama waliopendekezwa kuteuliwa kuwa madiwani wanawake wa viti maalum kama ifuatavyo:-

NA.	JINA	HALMASHAURI YA
1.	Ndg. Mecha Goodluck Matile	Halmashauri ya Jiji la Tanga
2.	Ndg. Joyce Milembe Aenda	Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe
3.	Ndg. Sharifa Hassan Magalagala	Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu
4.	Ndg. Clementina Daudi Mateja	Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa
5.	Ndg. Mariam Abdi Galu	Halmashauri ya Wilaya ya Chemba

Imetolewa na:


Mhailima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI